# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 44 Toba na ubatizo

**SOMA Warumi 6:3 – 5; Matendo 9:1 – 16; Luka 19:1 – 10; 1 Petro 3:21**

**SOMO**

Petro aliambia watu Yerusalemu, "Tubu na mbatizwe, kila mmoja wenu, katika jina la Yesu, kwa msamaha wa dhambi zenu." Kutubu ni kuachana na dhambi. Inamaanisha umekuwa ukiendelea kwa njia isiyonzuri. Usiende kwa njia zako mwenywe lakini ubadilike na uachane na dhambi na uanze kwenda kwa njia za Mungu.

Kubadilika utoke kwa dhambi na kumwendea Mungu ni vyema sana na ni uamuzi wa maana umefanya kwa maisha yako. Toba inamatokeo ya nguvu moyoni mwako, dhamiri yako, mawazo yako na hata kwa maisha yako yote.

Adamu na hawa walipofanya dhambi, walikuwa na uoga na wakajaribu kujificha kutoka kwa Mungu. Ukitubu, Mungu atakusamehe kila kitu. Mungu hufuta dhambi zako na unaanza upya. Mzigo wa dhambi na uoga inakuondokea kabisa.

Kutubu ni kuamua kubadilisha maisha yako. Tunamifano kwa Biblia ya watu waliotubu na kubadilisha maisha yao. Mtume Paulo alikuwa anatesa Wakristo. Hakuamini kwamba Yesu alikuwa kweli ni Mwana wa Mungu. Wakati Yesu alimwonekania njiani akienda Dameski, Paulo alijuta kuona kwamba alikuwa na makosa, alisikitika sana kwa yote aliyofanya. Alitubu na kubadilisha maisha yake na kuishi maisha ya kuhubiri Injili.

Zakayo alikuwa mtosha ushuru. Alikuwa mlafi, mchoyo na muongo. Lakini Yesu alipoenda kwa nyumba yake, alitubu. Zakayo aliaibikia dhambi zake sana na akabadilisha maisha yake. Alipea maskini nusu ya pesa yake na alilipa mara nne kwa yeyote aliyekuwa amemdanganya.

Kutubu inamaanisha ni kubadilisha maisha yako kabisa. Hii huwa ni vigumu kufanya, lakini inabidi. Unatakiwa ubadilike kwa kuondoa mambo yako mabaya ya zamani na kuweka mazuri.

### Maswali na Majibu

*1.* Nini maana ya 'kutubu'?
*Kabadilika na kuacha dhambi halafu utembee kwa njia za Mungu.*

*2.* Peana mfano ya watu wawili waliotubu na wakabadilisha maisha yao.
*Paulo na Zakayo.*

*3.* Ni mshahara gani tunastahili kupata kutoka kwa Mungu? *Kifo.*

*4.* Zawadi kuu yenye Mungu anataka atupe ni gani? *Uzima wa milele.*

*5.* Yesu ametuwezesha kupata wokovu namna gani?
*Kwa kupeana uhai wake uliyokamilifu msalabani ili sisi tupate msamaha wa dhambi?*

*6.* Tunahusishwa kwa kifo na kufufuka kwa Yesu wakati wa ubatizo namna gani?
*Tunazikwa kwa maji vile Yesu alizikwa alipokufa. Tunatoka ndani ya maji vile Yesu alifufuka kutoka kwa wafu.*

7. Mbona tubatizwe kwa kuzikwa ndani ya maji?
*Kwa sababu hiki ni kitendo kuonyesha kufa na kufufuka*.

*8.* Mbona kunyunyizia mtoto maji si ubatizo wa kweli?
*Mtoto hawezi kuamini au kutubu au kuahidi kumtumikia Mungu.*

9. Tunahitajika tufanye nini baada ya ubatizo?
*Tuanze maisha mapya ya kupenda na kumtumikia Mungu kwa maisha yetu yote*.

*10.* Unakuwa mtu wa familia gani baada ya kubatizwa? *Familia ya Mungu.*

### Mistari ya kukariri

Warumi 6:3 – 5; 1 Yohana 1:9 1 Petro 3:21

### Mazungumzo

Zungumza vile ubatizo unatakiwa ubadilishe maisha yako. Kwa hivyo mwenendo wako unatakiwa uwe wa namna gani kwa: familia yako, marafiki wako, kwa kazi/shule yako, wakati wako, maombi yako, malengo ya maisha yako, mfano wako kwa wengine?

### Kuandika

Chora ama uandike vile ubatizo unatuhusisha sisi na kifo na kufufuka kwa Yesu.

Sisi wote tuna mambo fulani yasiyomazuri katika maisha yetu. Tuna vitu tunakuwa na ugumu wa kubadilisha. Labda tuna hasira mbaya au tunapenda kusema uongo na hatufurahii. Kutubu ni kuendelea kujaribu kubadilika. Kitu cha maana ni kuendelea kuomba Mungu atusaidie. Ikiwa kweli tunataka kubadilika, Mungu atatusaidia.

Kutubu ni hatua ya kwanza kwa mtu yeyote anayetaka kuokoka. Tunatakiwa tuwe na msukumo wa kutaka Mungu kwa maisha yetu. Hii inatakiwa itoke moyoni mwetu. Hatuwezi kupata wokovu kwa juhudi yetu wenyewe. Mshahara tunaostahili kupata machoni mwa Mungu ni kukubali kwamba sisi ni wenye dhambi. Na hiyo ni kifo. Lakini Mungu anataka atupe uzima wa milele. Hii ndiyo zawadi kubwa kwetu. Mungu ameahidi uzima wa milele kwa wale watakaotubu na kubatizwa katika jina la Yesu Kristo. Tunatakiwa tumfuate Yesu kama wanafunzi wake. Tunatakiwa tuamue sisi wenyewe. Mungu anatuita tuamini Injili, tutubu na tubatizwe. Lakini hatulazimishwi kufanya hivyo.

Kushindana kwa maovu na mabaya kumekuweko tangu wakati Adamu na Hawa walikula tunda walilokataswa. Yesu ametushindia hivi vita. Alishida dhambi kupitia kwa kifo chake. Tunaweza tu, kuokoka kwa sababu Yesu alipeana uhai wake usiokuwa na makosa kwa msalaba ili tusamehewe dhambi zetu. Yesu alikufa kutuokoa kutoka dhambini. Tukibatizwa tunahusishwa kwa kifo na ufufuo wa Yesu. Tunahusishwa kukufa na kufufuka na kuanza maisha mapya.

**Kifo na kufufuka kwa Yesu**




**Tunahusishwa kwa kifo cha Yesu kupitia kwa ubatizo**




Kubatizwa ni kuzikwa ndani ya maji. Huu ni mfano wa kuzikwa. Tunakubali kwamba tunastahili kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Kuzikwa ndani ya maji ni mfano wa kufa na Kristo. Vile Yesu alitoka kaburini na sisi nasi tunatoka ndani ya maji kuanza maisha mapya katika Yesu.

Ubatizo ni kama kuoshwa. Sio kuoshwa kwa ngozi yetu chafu. Ni kuoshwa dhambi zetu. Tunaweza kuona ngozi yetu kama ni chafu lakini hatuwezi kuona dhambi zilizondani yetu. Tukitoka ndani ya maji baada ya ubatizo, hatuwezi kuona kwamba dhambi zetu zimeoshwa. Lakini hivi ndivyo Mungu anatuona. Tukisha batizwa, Mungu anatuona kama watu waliowasafi ndani, bila dhambi.

*Makanisa mengi 'wanabatiza' watoto kwa kuwanyunyizia maji. Huu si ubatizo wa Biblia. Kabla ya kubatizwa lazima mtu aamini kwa Yesu na nguvu za Mungu za msamaha wa dhambi. Lazima aamini kwa Ufalme wa Mungu ujao. Lazima atubu na aahidi kwamba atajaribu kumtumikia Mungu kwa maisha yake yote. Mtoto hawezi kufanya hayo yote.*

Kuamua kubatizwa ni jambo la maana lenye mtu anatakiwa afanye. Ni tendo la maisha. Inatakiwa mtu awe mwangalifu na afikirie sana. Inatakiwa aamue yeye mwenyewe.

Kabla ya ubatizo mtu anatakiwa aelewe na aamini mafundisho ya kweli ya Biblia. Halafu kuwe na kutubu dhambi zetu na haja ya kumtumikia Mungu maisha yote.

Kubatizwa ni mwanzo wa maisha mapya. Maisha ya zamani yanakufia kwa maji na mtu anatoka na anaanza maisha mapya kama mmoja wa wana wa Mungu. Bado tunatenda dhambi baada ya ubatizo lakini kwa vile ni watoto wa Mungu anatusamehe tukitubu hizo dhambi kupitia kwa Yesu. Mtu mwumini aliyebatizwa huwa anapigana na dhambi zake kujaribu kutii amri za Mungu. Kuna mabadiliko tunayotakiwa kufanya katika haya maisha mapya. Tunatakiwa tujaribu kila siku kuishi maisha yanayopendeza Mungu. ingawaje tuko na Baba wa upendo anatusaidia na Yesu ametuonyesha mfano uliomzuri usio na kasoro.

Ukibatizwa, unaunganishwa na familia ya Mungu. Unafurahi kuwa na Mungu wa upendo anayekujali na anatuongoza. Unatazamia kuwa na uzima wa milele kwa Ufalme wa Mungu. Mungu ametwambia kwamba anataka tuwe huko.